# MTU MWENYE UJUMBE

## Habari Kuu Kuwahi Kuambiwa

Habari zimekusanywa na kupangwa na
Gerhard Nehls

05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 1 27-05-2022 12:48:01

Kichwa cha asili cha kitabu: Man with a Message

© 2022, kwa Toleo la Kiswahili
Life Challenge
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**www.life-challenge.org**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa kunakiliwa bila idhini ya maandishi, isipokuwa kwa nukuu fupi katika vitabu na mapitio.

Nukuu zote za Kurani zimetolewa kwenye: KURANI TAKATIFU, iliyofasiriwa na Sheikh Abdullah Saleh Farsi, chapa ya saba, 1993.

Nukuu za Biblia zimetolewa kwenye: NENO BIBLIA TAKATIFU, 2014.

Kimetafsiriwa na John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania.

ISBN: 978-9966-895-78-3

Kimechapishwa nchini Kenya.

05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 2 27-05-2022 12:48:01

# Mtu Mwenye Ujumbe

Zamani barua zilichukua siku nyingi, wakati mwingine wiki kadhaa ama hata mwezi kabla zimfikie mlengwa. Siku hizo hakukuwa na barua pepe, mtandao wala simu za rununu. Hata huduma za Posta hazikuwepo jinsi tunavyozifahamu siku hizi. Hata hivyo, bado watu waliweza kupata njia za kuwasiliana na wenzao.

Ujumbe ulitumwa kupitia kwa mtu mmoja hadi mwingine. Ilifanyika pia kwamba ujumbe ulitumwa kutoka kwa Mungu kupitia kwa wajumbe hadi kwa wanadamu. Tunaamini kwamba Mungu amezungumza ili kuwasiliana na mwanadamu. Bila shaka tungetarajia kwamba aliyebuni na kuumba ulimwengu atajitambulisha yeye ni nani na atume maagizo jinsi ya kuishi kwa amani na yeye mwenyewe, Muumba wetu, sivyo!

Mtu aliyedai kwamba amepokea jumbe kutoka kwa Mungu, aliitwa “nabii”. Tafsiri halisi ya neno hili katika Kiarabu na Kiebrania, maana yake ni ‘mjumbe’.

Wayahudi, Wakristo na Waislamu, wote wanakubaliana kwa kiwango fulani, kwamba hao manabii walikuwa akina nani. Baadhi yao ni Nuhu, Ibrahimu, Musa, Eliya, Ayubu, na Daudi. Wayahudi watapinga kumpa Yesu cheo cha nabii huko Waislamu nao humwita Yesu, “Nabii Isa”.

Jambo la kushangaza ni kwamba ingawa Yesu anaitwa nabii, ujumbe wake haumo kwenye Kurani. Ujumbe wa Yesu unapatikana tu kwenye Injili.



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 1 27-05-2022 12:48:01

Inashangaza kuwa siku hizi walimu wa Kiislamu wanadai kwamba ujumbe wa Yesu ulinuiwa tu kwa Wayahudi pekee, ilhali Kurani inasema kwamba Yesu alikuwa “miujiza kwa walimwengu”, yaani, watu wote (Sura 21:91).

Kurani inafunza kwamba: “Tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahim, Ismail, Is-haqa, na Yaaqubu na kizazi chake ... na waliyopewa Musa na Isa na pia yale waliyopewa Manabii wengine. Hatutofautishi baina ya yo yote” (Sura 2:136).

Ili kuelezea pingamizi hii baina ya Kurani na Biblia, walimu wa Kiislamu hudai kwamba Biblia ya awali iliyokuwa na ujumbe wa “Ibrahimu ... Musa na Yesu” siyo Neno la Mungu bali imebadilishwa na kufanyiwa ubatili.

Lakini sivyo ifundishavyo Kurani inaposema, “Enyi watu wa Kitabu! Hamko juu ya cho chote, mpaka msimamishe Torati na Injili na hayo yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu” (Sura 5:68). Maneno haya yaliandikwa karne ya saba. Nakala za zamani za Biblia ambazo zingali ziko hadi sasa, ni nzee kuliko Kurani, lakini hazitofautiani na Biblia tuliyo nayo.

Kurani inawapa Waislamu changamoto ikisema: “Na kama unayo shaka juu ya hayo tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao vitabu kabla yako” (Sura 10:94). Je, ni kitabu kipi? Kile kilichokuja kabla ya Kurani? Hakuna mtu ye yote anayeweza kudai kwa kutumia Kurani kwamba Biblia imebadilishwa. Kurani inawaamuru Waislamu “waulizeni wenye kumbukumbu ya mambo ya zamani, ikiwa nyinyi hamjui” (Sura 21:7). Wenye kumbukumbu walikuwa Wayahudi na Wakristo.

Kama ambavyo tumeona, Kurani inasema wazi kwamba Injili ni Neno la Mungu. Pia inasema wazi wazi kwamba, “Hakuna mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu" (Sura 10:64 na 6:34)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 2 27-05-2022 12:48:01

Kwa kuwa ni watu wachache tu wanaojisomea Injili wenyewe, kijitabu hiki kimekusanya baadhi ya maneno aliyoyasema Yesu alipokuwa hapa duniani. Maneno hayo yameorodheshwa kulingana na kila hoja ili iwe rahisi kwa msomaji kuelewa. Yale yote ambayo yameandikwa kwa herufi za mlazo ni nukuu ya maneno aliyoyasema Yesu.



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 3 27-05-2022 12:48:01

## ALIYOSEMA YESU KUHUSU YEYE MWENYEWE

Ujumbe wake unatoka kwa Mungu na ukweli wake unaweza kuthibitishwa:

*Ndipo Yesu akawajibu, "Mafundisho yangu si yangu mwenyewe, bali yanatoka kwake yeye aliyenituma."*
(Yohana 7:16)

Ujumbe wake ni wa milele na kamwe hautabadilishwa:

*"Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe."* (Mathayo 24:35)

Alikuja duniani (yaani kutoka nje):

*"... Kwa kusudi hili nilizaliwa, na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Mtu yeyote aliye wa kweli husikia sauti yangu."* (Yohana 18:37)

Alikuja kutoka mbinguni, yaani kutoka kwa Mungu:

*"Hakuna mtu yeyote aliyekwenda mbinguni isipokuwa yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu."* (Yohana 3:13)

Daima Mungu alikuwa na Yesu:

*"Yeye aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha, kwa kuwa siku zote nafanya mapenzi yake."* (Yohana 8:29)

Yesu alikuwa na nia moja tu moyoni mwake, kumfurahisha na kumtukuza Baba yake wa mbinguni na kukamilisha kazi yake:

*Lakini Yesu akawajibu, "Chakula changu ni kufanya mapenzi ya Mungu ambaye amenituma na kuikamilisha kazi yake."* (Yohana 4:34)

Na kwa nini tumwamini?

*"Je, kuna yeyote miongoni mwenu awezaye kunithibitisha kuwa mwenye dhambi? Kama nawaambia yaliyo kweli, mbona hamniamini?"* (Yohana 8:46)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 4 27-05-2022 12:48:01

Waislamu hufundishwa kwamba manabii wote wa Mungu hawakutenda dhambi. Huu ni ubatili wa ukweli. Yesu pekee ndiye anatajwa kuwa hana dhambi au mtakatifu (Sura 19:19). Kwingineko tunasoma kuhusu dhambi za Adamu (Sura 7:22-23), Musa (Sura 28:15-16), Ibrahimu (Sura 26:82), Yunus (Sura 37:141- 144), Daudi (Sura 38:24-25), na pia hata Mohammed (Sura 40:55; 47:19; 48:1-2).

Ili sisi tuweze kufanya kazi ya Mungu, sharti tumwamini Yesu:

> *Yesu akawajibu, "Kazi ya Mungu ndiyo hii: Mwaminini yeye aliyetumwa naye."* (Yohana 6:29)

Kumkana Yesu ni kumkana Mungu!

> *"Yeye awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi; naye awakataaye ninyi amenikataa mimi. Lakini yeye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma."* (Luka 10:16)

Yesu hakuja tu kuleta ujumbe, bali kutimiza jukumu:

> *"Kwa maana Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."* (Luka 19:10)

Alikuja kuwaita wenye dhambi watubu na kuwaokoa kutoka jehanam. Wale wanaojiona kuwa ni wazuri na wanastahili kuingia kwenye uwepo wa Mungu, hujiona kuwa hawahitaji Yesu:

> *Yesu aliposikia haya akawaambia, "Watu wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."* (Marko 2:17)

Kwa wachovu anakuwa kama ndugu. Anataka kuleta amani kwa mioyo iliyodhoofika:

> *"Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi."* (Mathayo 11:28-30)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 5 27-05-2022 12:48:01

Maji yahitajika kwa uhai. Kuongea kiroho, Yesu anatoa "maji ya uzima" si tu ili kutosheleza mahitaji yetu, lakini ili sisi pia tuwe chemichemi na wengine wanywe pia:

*Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu, wakati Yesu akiwa amesimama huko, akapaza sauti yake akasema, "Kama mtu yeyote anaona kiu na aje kwangu anywe."*

(Yohana 7:37)

*"Lakini yeyote anywaye maji nitakayompa, hataona kiu kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa milele."*

(Yohana 4:14)

Kumkubali Yesu jinsi alivyo ni thibitisho kwamba tunampenda Mungu:

*"Lakini ninajua kwamba hamna upendo wa Mungu mioyoni mwenu. Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, nanyi hamnipokei, lakini mtu mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea."* (Yohana 5:42-43)

Kulingana na desturi za nyakati hizo, mara nyingi Yesu alizungumza juu yake mwenyewe katika nafsi ya tatu kana kwamba anazungumza kuhusu mtu mwingine. Kuongea hivyo, Yesu anatoa dai kubwa juu yake mwenyewe:

*"Yeyote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Kwa kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe. Lakini yule aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru, ili ionekane wazi kwamba matendo yake yametendeka katika Mungu."*

(Yohana 3:18-21)

*"Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu yeyote akinifuata*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 6 27-05-2022 12:48:01

*hatatembea gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima."* (Yohana 8:12)

*"Yeyote aniaminiye, haniamini mimi peke yangu, bali yeye aliyenituma. Yeyote anionaye mimi, amemwona yeye aliyenituma. Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni, ili kwamba kila mtu aniaminiye asibaki gizani."*

(Yohana 12:44-46)

Mara nyingi Yesu alizungumza kwa mafumbo na mifano. Hapa anazungumza kuwa yeye ni mlango na mchungaji, na wafuasi wake ni kondoo:

*"Mimi ndimi lango, yeyote anayeingia zizini kwa kupitia kwangu ataokoka, ataingia na kutoka, naye atapata malisho. Mwizi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao tele."*

(Yohana 10:9-10)

*"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo."* (Yohana 10:11)

*"Akiisha kuwatoa wote nje, hutangulia mbele yao na kondoo humfuata kwa kuwa wanaijua sauti yake."*

(Yohana 10:4)

Huko *"kutoa uhai wake"* kilikuwa kitendo cha hiari kulingana na mamlaka yake

*"Baba yangu ananipenda kwa kuwa ninautoa uhai wangu ili niupate tena."* (Yohana 10:17)

Uzima kamili ambao Yesu alikuja kuleta unajumuisha hakikisho la sasa na maisha yajayo:

*"Kondoo wangu huisikia sauti yangu nami nawajua, nao hunifuata, nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka mikono yangu. Baba yangu aliyenipa hawa ni mkuu kuliko wote na hakuna awezaye*

*kuwapokonya kutoka mikononi mwake. Mimi na Baba yangu tu umoja."* (Yohana 10:27-30)

Kwa mtu ambaye ndugu yake alikuwa kaburini kwa siku tatu, kisha akafufuliwa kutoka wafu na Yesu, alisema:

*Yesu akamwambia, "Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi, hata akifa atakuwa anaishi na yeyote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki haya?"* (Yohana 11:25-26)

Yesu aliweka wazi kwamba yeye tu ndiye njia ya pekee ya wokovu wa milele:

*Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu."* (Yohana 14:6)

Wakati mwingine Yesu alitumia vilinganishi kuelezea mambo ya kiroho. Moja kati ya hivyo ni dhahiri sana. Kwa hicho kilinganishi, anaelezea kule alikotoka na sababu yake ya kuja duniani:

*"Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima."* (Yohana 6:33)

*"Mimi ndimi mkate wa uzima. Yeye ajaye kwangu, hataona njaa kamwe na yeye aniaminiye, hataona kiu kamwe."* (Yohana 6:35)

*"Wale wote anipao Baba watakuja kwangu na yeyote ajaye kwangu, sitamfukuzia nje kamwe. Kwa kuwa nimeshuka kutoka mbinguni si ili kufanya mapenzi yangu, bali mapenzi yake yeye aliyenituma. Haya ndiyo mapenzi yake yeye aliyenituma, kwamba, nisimpoteze hata mmoja wa wale alionipa, bali niwafufue siku ya mwisho."* (Yohana 6:37-39)

*"Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima."* (Yohana 6:63)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 8 27-05-2022 12:48:01

Hapa Yesu anabainisha wazi kuwa:

*"Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja kwa ajili yangu mwenyewe, ila yeye alinituma."*

(Yohana 8:42)

*Akawaambia, "Ninyi mmetoka chini, mimi nimetoka juu. Ninyi ni wa ulimwengu huu, mimi si wa ulimwengu huu. Niliwaambia kuwa mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa katika dhambi zenu."* (Yohana 8:23-24)

Kabla ya kifo chake, Yesu alizungumza na wafuasi wake wa karibu akiwaambia:

*"Nilitoka kwa Baba na kuja ulimwenguni, sasa naondoka ulimwenguni na kurudi kwa Baba."* (Yohana 16:28)

Aliwahimiza wafuasi wake waamini uungu wake na akafafanua dai lake hivi:

*"Yeyote aliyeniona mimi, amemwona Baba!"*

(Yohana 14:9)

*"Nisadiki mimi kwamba niko ndani ya Baba na Baba yuko ndani yangu, la sivyo, niaminini kwa sababu ya zile kazi nizitendazo."* (Yohana 14:11)

Kwenye maombi yaliyonakiliwa Yesu alizungumza na Baba yake na kuongea kuhusu uwepo wake wa milele:

*"Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja na wewe kabla ulimwengu haujakuwepo."* (Yohana 17:5)

Kwa kuwa Yesu alikuwa na mama mwanadamu, alionekana kama mwanadamu wa kawaida, na kweli alikuwa mwanadamu. Kama sisi tulivyo, alihisi njaa na hata kuchoka, alihitaji kuomba, alihuzunika na kuhisi uchungu. Lakini kwa kuwa Mungu alikuwa amempa uvuvio na kuzaliwa kwake kukawa bila baba wa



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 9 27-05-2022 12:48:01

kibinadamu, alikuwa na uungu. Aliweza kuponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kutembea kwenye maji, kusamehe dhambi, kutuliza dhoruba, na kutenda miujiza mingine mingi. Kwa hiyo aliweza kudai uhusiano kati yake na Mungu ambao mwanzoni huenda ukatushangaza:

> *Wote wakauliza, "Wewe basi ndiwe Mwana wa Mungu?"Yeye akawajibu, "Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye."* (Luka 22:70)

Uhuru kutokana na woga, hata woga wa kifo, mashambulizi ya kishetani na uhuru kutokana na dhambi, unapatikana tu kwake peke yake:

> *"Hivyo Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli."* (Yohana 8:36)

Siku moja Yesu alitoa tamko la ajabu kuhusu yeye mwenyewe. Je, tunaweza kuelewa alichomaanisha? Wasikilizaji wake walimwelewa!

> *Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaambia, kabla Ibrahimu hajakuwako, 'Mimi niko.' "* (Yohana 8:58)

Ni muhimu kufahamu kwamba katika Kiebrania, neno "nipo" ni sawa na "Yahweh", jina halisi la Mungu! Jambo hili liliwafanya Wayahudi watake kumwua Yesu. Hapa tunapata ushahidi zaidi. Kwa kuwa Mungu ni wa milele, kwake hamna "nili" wala "nita". Daima yeye "ni". Alichokimaanisha ni kwamba: 'Kabla Ibrahimu kuwepo, nilikuwepo milele!"

Hata hivyo hayupo kule mbinguni bila kutujali. Anakupenda wewe na mimi! Anatutaka tuitikie huu upendo!

> *"Kama vile Baba alivyonipenda mimi, hivyo ndivyo mimi nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni katika pendo langu."*
> (Yohana 15:9)

Upendo wake unazidi ule wa kihisia tu. Alithibitisha upendo wake!



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 10 27-05-2022 12:48:01

> *"Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake."* (Yohana 15:13)

Mara kadhaa Yesu alizungumzia kuhusu kifo chake kilichokuwa kinakaribia na lengo la kufa kwake:

> *"... kama vile ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi."* (Mathayo 20:28)

Siku hizi neno 'fidia' halitumiki sana. Wakati mwingine tunasoma kuhusu watekaji nyara wakidai fidia. Haya ni malipo ambayo hudaiwa ile mateka waachiliwe huru. Yesu alilipa malipo ya kutuweka huru kutokana na hukumu ya dhambi.

Mara nne Yesu alitabiri kifo chake kwa wafuasi wake wa karibu. Lakini hata kwao, mwanzoni utabiri huo haukuwa na maana:

> *Akasema, "Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atasalitiwa kwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria. Wao watamhukumu kifo na kumtia mikononi mwa watu wa Mataifa, ambao watamdhihaki na kumtemea mate, watampiga na kumuua. Siku tatu baadaye atafufuka."* (Marko 10:33-34)

Kabla ya kifo chake Yesu alidhoofika katika maombi, akifikiria kuhusu mateso, uchungu na mateso ya msalaba yaliyokaribia:

> *Akaenda tena mara ya pili na kuomba, "Baba yangu, kama haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisikinywe, basi mapenzi yako yafanyike."* (Mathayo 26:42)

Halikuwa kundi la wasiomjua Mungu lililotaka kumkamata. Walikuwa viongozi wakuu wa kidini wa siku hizo, na waliogopa kwamba mamlaka yao yalikuwa yametishiwa na Yesu. Alipokamatwa, mmoja wa wafuasi wake alichomoa upanga akitaka kupigana. Lakini Yesu akasema:

> *"Je, unadhani siwezi kumwomba Baba yangu naye mara moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 11 27-05-2022 12:48:01

*malaika? Lakini je, yale Maandiko yanayotabiri kwamba ni lazima itendeke hivi yatatimiaje?"* (Mathayo 26:53-54)

Ili kuelewa maneno "yatatimiaje Maandiko" inabidi tufahamu kwamba manabii wa Agano la Kale mamia ya miaka iliyopita walikuwa wametabiri matukio makuu katika maisha ya Yesu. Kuwepo kwake tangu milele, kuzaliwa kwake kimiujiza na bikira na uungu wake, kifo chake msalabani na kufufuka kwake kutoka wafu, yote yalikuwa yamenakiliwa. Katika Yesu, hayo yote yalitimizwa.

Dai la uungu wa Yesu liliwachukiza Wayahudi kama linavyowachukiza watu hata na siku hizi:

*Kwa mara nyingine Wayahudi wakainua mawe ili wampige nayo, lakini Yesu akawaambia, "Nimewaonyesha miujiza mingi mikubwa kutoka kwa Baba yangu. Ni ipi katika hiyo mnataka kunipiga mawe?" Wayahudi wakamjibu, "Hatukupigi mawe kwa sababu ya mambo mema uliyotenda, bali ni kwa kuwa umekufuru. Wewe ingawa ni mwanadamu unajifanya kuwa Mungu."*

(Yohana 10:31-33)

Hata wakati huu wa mahangaiko katika maisha yake, Yesu hakufikiria sana kuhusu yeye, bali alifikiria kuhusu wengine:

*Walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, hapo ndipo walipomsulubisha Yesu pamoja na hao wahalifu, mmoja upande wake wa kuume na mwingine upande wake wa kushoto. Yesu akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!" Wakagawana nguo zake kwa kupiga kura.* (Luka 23:33-34)

Baada ya kufufuka kwake kutoka wafu Yesu alijiunga na baadhi ya wafuasi wake wakielekea nyumbani, lakini kwa muda hawakuweza kumtambua. Walikuwa na huzuni mwingi kutokana na kifo chake ambacho hawakuweza kuelewa. Yesu akawaambia:



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 12 27-05-2022 12:48:01

*"Ninyi ni wajinga kiasi gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu kuamini mambo yote yaliyonenwa na manabii! Je, haikumpasa Kristo kuteswa kwa njia hiyo na kisha aingie katika utukufu wake?" Naye akianzia na Sheria ya Mose na Manabii wote, akawafafanulia jinsi Maandiko yalivyosema kumhusu yeye.* (Luka 24:25-27)

Kwa mara nyingine Yesu aliwaelekeza kwa unabii wa Agano la Kale kumhusu yeye mwenyewe:

Kuna watu ambao wamedai kuwa Yesu hakufa, bali alitolewa msalabani akiwa amezirai na baadaye akapata tena fahamu. Hili halingewezekana kamwe, kwani ili askari wathibitishe kuwa amekufa, walimdunga mkuki kifuani mwake kabla ya kuutoa mwili wake msalabani (Yohana 19:33). Je, Yesu mwenyewe alisemaje kuhusu kifo chake?

*"... Mimi ndiye wa Kwanza na wa Mwisho. Mimi ni Yeye Aliye Hai, niliyekuwa nimekufa, na tazama, ni hai milele na milele! Nami ninazo funguo za mauti na kuzimu."*
(Ufunuo wa Yohana 1:17-18)

Yesu hakuja kwa ajili ya Wayahudi pekee kama wanavyodai watu wengine:

*Akawaambia, "Haya ndiyo yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. Toba na msamaha wa dhambi zitatangaziwa mataifa yote kupitia jina lake kuanzia Yerusalemu.* ( Luka 24:46-47)

Baada ya kufufuka kwake kutoka wafu, Yesu aliwahakikishia wanafunza wake kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, kisha akanyanyuliwa hadi mbinguni mbele ya macho yao. Maneno yake ya mwisho yalikuwa:

*"... Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu ... "* (Mathayo 28:18-20)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 13 27-05-2022 12:48:01

Wakristo kusukumwa mioyoni mwao na shauku ya kumjulisha Yesu na ujumbe wake. Mwisho utakapofika, Yesu ndiye atakuwa hakimu:

*"Hakika kama vile Baba awafufuavyo wafu na kuwapa uzima, vivyo hivyo Mwana huwapa uzima wale anaopenda. Wala Baba hamhukumu mtu yeyote, lakini hukumu yote amempa Mwana, ili wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Yeyote asiyemheshimu Mwana, hamheshimu Baba aliyemtuma.*
*Amin, amin nawaambia, yeyote anayesikia maneno yangu na kumwamini yeye aliyenituma, anao uzima wa milele, naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka mautini, na kuingia uzimani. Amin, amin nawaambia, saa yaja, nayo saa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, nao watakaoisikia watakuwa hai. Kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani yake. Naye amempa Mwanawe mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa yeye ni Mwana wa Adamu.*
*Msishangae kusikia haya, kwa maana saa inakuja ambapo wale walio makaburini wataisikia sauti yake."*

(Yohana 5:21-28)

Hata kama hakuna kitu kingine cha kutufanya tufikirie na tutafakari – jambo hili lazima litufanye tutafakari! Kukataa mwito huu kwa sababu ya woga fulani ni ujinga.

Yesu anatuhimiza tumtegemee yeye na yote anayotutendea:

*Yesu akawaambia, "Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi pia. Nyumbani kwa Baba yangu kuna makao mengi. Kama sivyo, ningeliwaambia. Naenda kuwaandalia makao. Nami nikienda na kuwaandalia makao, nitarudi tena na kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali nilipo, nanyi mpate kuwepo."* (Yohana 14:1-3)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 14 27-05-2022 12:48:01

Yesu atarudi tena. Lakini wakati huo hatakuja kuokoa bali kuwahukumu wale wote ambao hawakukubali mwito wake wa msamaha. Kwa hiyo ni muhimu kuwa tayari wakati wo wote kwa kuja kwake:

*"Ninyi nanyi hamna budi kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja saa msiyotazamia."* (Luka 12:40)

Jinsi mambo haya yatakavyofanyika, pia alituambia:

*"Nanyi mtamwona Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mwenye Nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni." (*Marko 14:62)

*"Kwa maana kama vile umeme utokeavyo mashariki na kuonekana hata magharibi, ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."* (Mathayo 24:27)

Yesu anarudi tena kuhukumu ulimwengu – mataifa na watu wote. Lakini huenda wengine wetu tutakufa kabla ya kuja kwake. Kama ni hivyo, tunakutana naye pale tunapokufa.

Kwa nini Yesu anajiita *'Mwana wa Adamu'* na si 'Mwana wa Mungu'? Sifa hii *'Mwana wa Adamu'* imetajwa mara ya kwanza katika Agano la Kale mwaka wa 555 kK.

*"Katika maono yangu ya usiku nilitazama, na mbele yangu nikamwona anayefanana na mwanadamu, akija pamoja na mawingu ya mbinguni. Akamkaribia huyo Mzee wa Siku, na akaongozwa mbele zake. Akapewa mamlaka, utukufu na ufalme wenye nguvu; nao watu wa kabila zote, mataifa, na watu wa kila lugha wakamwabudu. Utawala wake ni utawala wa milele ambao hautapita, nao ufalme wake ni ule ambao kamwe hautaangamizwa."*

(Danieli 7:13-14)

Kutokana na usemi huu tunaona kwamba hakuna tofauti kati ya *'Mwana wa Adamu'* na 'Mwana wa Mungu'.

Muda wa kupokea msamaha ungalipo. Yesu bado anangoja. Alituachia mwaliko:



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 15 27-05-2022 12:48:01

*"Tazama! Nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu yeyote akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye, naye pamoja nami."* (Ufunuo 3:20)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 16 27-05-2022 12:48:01

## YALE AMBAYO YESU ALITUFUNDISHA

Yesu hakufunza theolojia wala falsafa ya juu. Alizungumza na watu kadiri walivyoweza kuelewa:

> *Ndipo akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema: "Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake. Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine zilianguka kando ya njia, nao ndege wakaja na kuzila. Nyingine zilianguka kwenye ardhi yenye mwamba isiyo na udongo wa kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo ulikuwa haba. Lakini jua lilipozidi, mimea ikanyauka na kukauka kwa kuwa mizizi yake haikuwa na kina. Mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba, nayo miiba hiyo ikakua, ikaisonga hiyo mimea. Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri ambapo zilitoa mazao, nyingine mara mia moja, nyingine mara sitini, na nyingine mara thelathini. Mwenye masikio ya kusikia, na asikie."* (Mathayo 13:3-9)

> *"Sikilizeni basi maana ya ule mfano wa mpanzi: Mtu yeyote anaposikia neno la Ufalme naye asilielewe, yule mwovu huja na kunyakua kile kilichopandwa moyoni mwake. Hii ndiyo ile mbegu iliyopandwa kando ya njia. Ile mbegu iliyopandwa kwenye sehemu yenye mawe ni mtu yule ambaye hulisikia neno na mara hulipokea kwa furaha. Lakini kwa kuwa hana mizizi yenye kina ndani yake, lile neno hudumu kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki au mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, yeye mara huchukizwa. Ile mbegu iliyopandwa katika miiba ni yule mtu alisikiaye neno, lakini masumbufu ya maisha haya na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno na kulifanya lisizae matunda. Lakini ile mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri ni yule mtu ambaye hulisikia neno na kulielewa. Naye hakika huzaa matunda, akizaa mara mia, au mara sitini, au mara thelathini ya mbegu iliyopandwa."* (Mathayo 13:18-23)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 17 27-05-2022 12:48:01

Mungu aliwakemea wasikilizaji kwa kutoitikia ujumbe wake. Kwa hiyo Yesu akawaonya:

*"Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa; na pia mtatazama lakini hamtaona. Kwa kuwa mioyo ya watu hawa imekuwa migumu; hawasikii kwa masikio yao, na wamefumba macho yao. Wasije wakaona kwa macho yao, na wakasikiliza kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, na kugeuka nami nikawaponya."* (Mathayo 13:14-15)

*"Kwa hiyo, kuweni waangalifu mnavyosikia. Kwa maana yeyote aliye na kitu atapewa zaidi. Lakini yule asiye na kitu, hata kile anachodhani anacho atanyang'anywa."*
(Luka 8:18)

Katika mfano mwingine, Yesu alielezea ukweli muhimu:

*Kisha Yesu akawaambia mfano huu: "Mtu mmoja alikuwa na mtini uliopandwa katika shamba lake la mizabibu, akaja ili kutafuta tini kwenye mti huo, lakini hakupata hata moja. Hivyo akamwambia mtunza shamba: 'Tazama, kwa muda wa miaka mitatu sasa nimekuwa nikija kutafuta matunda kwenye mtini huu, nami sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini uendelee kuharibu ardhi?'*
*"Yule mtunza shamba akamjibu, 'Bwana, uache tena kwa mwaka mmoja zaidi, nami nitaupalilia na kuuwekea mbolea. Kama ukizaa matunda mwaka ujao, vyema, la sivyo uukate.'"* (Luka 13:6-9)

Katika mfano mwingine Yesu alieleza hivi:

"*Mimi ndimi mzabibu wa kweli na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo, hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililonena nanyi. Kaeni ndani yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa ndani ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi msipokaa ndani yangu hamwezi kuzaa matunda.*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 18 27-05-2022 12:48:01

*Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi. Akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana, maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya jambo lolote. Mtu yeyote asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka. Matawi kama hayo hukusanywa na kutupwa motoni, yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote mtakalo, nanyi mtatendewa. Kwa hiyo Baba yangu hutukuzwa, kwa vile mzaavyo matunda mengi, nanyi mtakuwa wanafunzi wangu."*

(Yohana 15:1-8)

Hakuna mmoja wetu anayeweza kudai kuleta matunda haya kwa bidii yake mwenyewe. Kwingineko katika Biblia tunaambia kwamba tunda ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminivu, upole, kiasi (Wagalatia 5:23). Nani hangependa kuzaa matunda haya?

Mfano mwingine unaelezea zaidi jambo hili:

*Yesu akaendelea kusema: "Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa na wana wawili. Yule mdogo akamwambia baba yake, 'Baba, nipe urithi wangu.' Hivyo akawagawia wanawe mali yake.*

*Baada ya muda mfupi, yule mdogo akakusanya vitu vyote alivyokuwa navyo, akaenda nchi ya mbali, na huko akaitapanya mali yake kwa maisha ya anasa. Baada ya kutumia kila kitu alichokuwa nacho, kukawa na njaa kali katika nchi ile yote, naye akawa hana chochote. Kwa hiyo akaenda akaajiriwa na mwenyeji mmoja wa nchi ile ambaye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akatamani kujishibisha kwa maganda waliyokula wale nguruwe, wala hakuna mtu aliyempa chochote.*

*Lakini alipozingatia moyoni mwake, akasema, 'Ni watumishi wangapi walioajiriwa na baba yangu ambao wana chakula cha kuwatosha na kusaza, bali mimi hapa nakufa kwa njaa! Nitaondoka na kurudi kwa baba yangu*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 19 27-05-2022 12:48:01

*na kumwambia: Baba, nimetenda dhambi mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili tena kuitwa mwanao; nifanye kama mmoja wa watumishi wako.' Basi akaondoka, akaenda kwa baba yake.*

*Lakini alipokuwa bado yuko mbali, baba yake akamwona, moyo wake ukajawa na huruma. Akamkimbilia mwanawe, akamkumbatia na kumbusu.*

*Yule mwana akamwambia baba yake, 'Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili kuitwa mwanao tena.'*

*Lakini baba yake akawaambia watumishi, 'Leteni upesi joho lililo bora sana, tieni pete kidoleni mwake na viatu miguuni mwake. Leteni ndama aliyenona, mkamchinje ili tuwe na karamu, tule na kufurahi. Kwa maana huyu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai tena; alikuwa amepotea na sasa amepatikana!' Nao wakaanza kufanya tafrija."* (Luka 15:11-24)

Tunahitaji 'kuzingatia mioyoni mwetu' kama alivyofanya mwana mpotevu. Hakujaribu kufidia matendo yake maovu kwa kujaribu kutoa malipo, ambayo hakuwa nayo. Baba yake hakutarajia malipo. Alitaka tu kurudi nyumbani – na akaenda. '*joho lililo bora*' ni mfano wa kufunika uchafu, pete ni ishara ya kukubaliwa tena kama mwana katika jamii, viatu navyo ni ishara kwamba yu huru tena, kwani watumwa walitembea bila viatu. Utaratibu huu ni sawa kama inavyofundishwa katika mfano mwingine:

*"Palikuwa na mtu mmoja aliyewakopesha watu wawili fedha: Mmoja alidaiwa dinari 500 na mwingine dinari hamsini. Wote wawili walipokuwa hawawezi kulipa, aliyafuta madeni yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao atakayempenda yule aliyewasamehe zaidi?"*

(Luka 7:41-42)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 20 27-05-2022 12:48:01

Msamaha ni kipawa kutoka kwa Mungu kwa wale wanaoutafuta na kuuomba kwa dhati. Habari zinazoashiria huruma ya Mungu zimerudiwa tena na tena:

> *Ndipo Yesu akawaambia mfano huu: "Ikiwa mmoja wenu ana kondoo mia moja, naye akapoteza mmoja wao, je, hawaachi wale tisini na tisa nyikani na kwenda kumtafuta huyo aliyepotea mpaka ampate? Naye akishampata, humbeba mabegani mwake kwa furaha na kwenda nyumbani. Kisha huwaita rafiki zake na majirani, na kuwaambia, 'Furahini pamoja nami; nimempata kondoo wangu aliyepotea.' Nawaambieni, vivyo hivyo kutakuwa na furaha zaidi mbinguni kwa sababu ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya kutubu."* (Luka 15:3-7)

Labda wengi wetu hatujawahi kumtazama Mungu kwa mwanga huu. Tunafikiri kwamba tunahitaji kumfidia Mungu kwa dhambi tulizotenda. Ilhali anachotaka ni moyo wetu. Kumbuka kwamba hata mmoja wa hao waliokuwa wanadaiwa aliweza kulipa. Dhambi inapotendwa, haiwezi kurekebishwa. Huko ni kutokuelewa hata kidogo utakatifu wa Mungu. Matokeo ya dhambi zetu ni mwanya mkubwa sana usio na daraja kati yetu na Mungu. Tunategemea tu yale ambayo Mungu anatufanyia! Hebu tutazame mfano wa mwisho ili tusikie ana yapi ya kusema kuhusu swala hili:

> "*Watu wawili walikwenda Hekaluni kusali, mmoja wao alikuwa Farisayo na mwingine alikuwa mtoza ushuru. Yule Farisayo, akasimama, akasali hivi na kuomba kwake mwenyewe: 'Mungu, nakushukuru kwa sababu mimi si kama watu wengine ambao ni wanyang'anyi, wadhalimu, na wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma, na natoa sehemu ya kumi ya mapato yangu.'*
>
> *Lakini yule mtoza ushuru akasimama mbali, wala*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 21 27-05-2022 12:48:01

*hakuthubutu hata kuinua uso wake kutazama mbinguni, bali alijipigapiga kifuani na kusema: 'Mungu, nihurumie, mimi mwenye dhambi.'*
*Nawaambia, huyu mtoza ushuru alirudi nyumbani akiwa amehesabiwa haki mbele za Mungu zaidi ya yule Farisayo. Kwa maana yeyote ajikwezaye atashushwa, na yeyote ajishushaye atakwezwa."* (Luka 18:10-14)

Mfarisayo alikuwa kiongozi wa kidini aliyeheshimika sana katika jamii siku hizo. Alizingatia kwa dhati maisha ya nidhamu ya juu katika juhudi za kutovunja hata moja ya sheria za Mungu. Lakini katika hali ya kujidanganya, alijitukuza katika mafanikio yake, kufunga kwake, matoleo yake, nk., akifikiri kwamba hayo yatamfanya akubaliwe na Mungu.

Yesu alieleza hivi:

*"Vivyo hivyo nanyi mkiisha kufanya mliyoagizwa, semeni, 'Sisi tu watumishi tusiostahili; tumefanya tu yale tuliyopaswa kufanya.'"* (Luka 17:10)

Yesu alisema kwamba hatustahili faida yo yote kwa kutenda sawa ama vizuri. Tunatarajiwa tutende mema, hilo ni jukumu letu kwa Mungu. Kiwango cha Mungu ndicho kanuni. Kwa hiyo, msamaha kwa kutotenda ipasavyo wakati wote ni neema ya Mungu. Ni kitendo cha msamaha ambacho hatustahili:

*Yesu akawaambia, "Ninyi mnajionyesha kuwa wenye haki mbele za wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa maana vile vitu ambavyo wanadamu wanavithamini sana, kwa Mungu ni machukizo."* (Luka 16:15)

Yesu alipoulizwa kuhusu ile amri kuu, alijibu:

*Yesu akamjibu, " 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote.' Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Nayo ya pili ni kama hiyo, nayo ni hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Amri hizi mbili ndizo msingi wa Sheria na Manabii."*
(Mathayo 22:37-40)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 22 27-05-2022 12:48:01

Maana ya kijeshi ya neno 'kutii' inatolewa makali yake, mtu anapotii kwa upendo!

Ingawa Yesu alitufundisha tumpende na tumwogope Mungu, alitufunza pia tusiogope yale ambayo wanadamu wanaweza kusema na kutendea:

> *"Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua roho. Afadhali mwogopeni yeye awezaye kuiangamiza roho na mwili katika jehanamu."* (Mathayo 10:28)

Pale tu tunapoiweka imani yetu kwa kile anachosema, na tunapomtumikia kwa mioyo yetu yote, ndipo tunamtukuza:

> *"... kwa maana Baba mwenyewe anawapenda, kwa sababu mmenipenda mimi na mmeamini kwamba nimetoka kwa Mungu."* (Yohana 16:27)

> *"Mtu yeyote akinitumikia lazima anifuate, nami mahali nilipo ndipo mtumishi wangu atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba yangu atamheshimu."* (Yohana 12:26)

Imani katika Mungu imeambatana na imani katika Yesu. Kwa kawaida, hakuna tofauti:

> *Yesu akapaza sauti akasema, "Yeyote aniaminiye, haniamini mimi peke yangu, bali yeye aliyenituma. Yeyote anionaye mimi, amemwona yeye aliyenituma. Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni, ili kwamba kila mtu aniaminiye asibaki gizani."* (Yohana 12:44-46)

> *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kupitia kwake ulimwengu upate kuokolewa."*
> (Yohana 3:16-17)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 23 27-05-2022 12:48:01

*“Kwa maana mapenzi ya Baba yangu ni kwamba kila mmoja amtazamaye, Mwana na kumwamini awe na uzima wa milele, nami nitawafufua siku ya mwisho.”*

(Yohana 6:40)

*“Kwa maana Baba mwenyewe anawapenda, kwa sababu mmenipenda mimi na mmeamini kwamba nimetoka kwa Mungu.”* (Yohana 16:27)

Uamuzi wote tunaoufanya una faida na madhara yake. Hii ni pamoja na uamuzi wa kumfuata Yesu. Huenda tukadhihakiwa na hata kuteswa:

*“Watu wote watawachukia kwa ajili ya Jina langu. Lakini yule atakayevumilia hadi mwisho ataokolewa.”*

(Mathayo 10:22)

*“Kumbukeni lile neno nililowaambia, ‘Hakuna mtumishi aliye mkuu kuliko bwana wake.’ Kama wamenitesa mimi, nanyi pia watawatesa. Kama wamelishika neno langu, watalishika na neno lenu pia.”* (Yohana 15:20)

Lakini Yesu anatufariji:

*“Heri ninyi watu watakapowashutumu, na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu. Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa kuwa hivyo ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwa kabla yenu.”* (Mathayo 5:11-12)

Yesu anataka tumpende, tumheshimu na tumtukuze yeye kuliko mtu mwingine au kitu kingine kile:

*“Yeyote ampendaye baba yake au mama yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili kuwa wangu. Yeyote ampendaye mwanawe au binti yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili kuwa wangu.”* (Mathayo 10:37)

Kama wana wa Mungu (yeye ni Baba yetu), na kwa sababu tunahitaji kuchukuliana sisi kwa sisi katika kutembea kwetu na Mungu, Yesu alisema:



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 24 27-05-2022 12:48:01

*"Amri mpya nawapa: Mpendane kama mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane."*

(Yohana 13:34)

Pia alituachia kipimo, ili tuweze kujipima sisi wenyewe:

*"Yeyote mwenye amri zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."* (Yohana 14:21)

Sisi ni watiifu kwa sababu tunamwamini na kumpenda. Lakini utiifu si chombo cha kutufanya tustahili msamaha na Paradiso.

Ufalme wa Mungu ni wa aina tofauti, na maana ya ukubwa unapimwa kwa viwango tofauti:

*Lakini Yesu akawaita wote pamoja na kuwaambia, "Mnafahamu kuwa watawala wa watu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao. Isiwe hivyo kwenu. Badala yake, yeyote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu ..."* (Mathayo 20:25-27)

Vile vile matendo ya kidini hudhihirishwa na kurekebishwa na Yesu:

*Yesu akaita tena ule umati wa watu, akawaambia, "Nisikilizeni, kila mmoja wenu na mwelewe jambo hili. Hakuna kitu kinachomwingia mtu kimtiacho unajisi, lakini kile kimtokacho ndicho kimtiacho unajisi."*

(Marko 7:14-15)

*Akawajibu, "Je, hata nanyi hamwelewi? Je, hamfahamu kwamba kitu kimwingiacho mtu hakimtii unajisi? Mtu akila kitu hakiingii moyoni mwake bali tumboni, na baadaye hutolewa nje ya mwili wake." (Kwa kusema hivi, Yesu alivihalalisha vyakula vyote kuwa ni "safi.")*
*Akaendelea kusema, "Kile kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. Kwa maana kutoka ndani ya moyo*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 25 27-05-2022 12:48:01

*wa mtu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wizi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, uovu, udanganyifu, ufisadi, wivu, matukano, kiburi na upumbavu. Maovu haya yote hutoka ndani ya mtu, nayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi."*

(Marko 7:18-23)

Hii ndiyo sababu Yesu aliwakemea viongozi wa kidini:

*"Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnasafisha kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. Ewe Farisayo kipofu! Safisha ndani ya kikombe na sahani kwanza, ndipo nje itakuwa safi pia."*

(Mathayo 23:25-26)

Matendo ya kidini hujihusisha mara nyingi na masuala ya vyakula na tambiko za kujitakaza. Haya ni kinyume kabisa na yale aliyofunza Yesu:

*"Heri walio na moyo safi, maana hao watamwona Mungu."*

(Mathayo 5:8)

Yesu anazungumzia mambo kadhaa kuhusu uhusiano wa kibinadamu na uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu. Maneno yake yanastahili yachome akili na mioyo yetu:

**Kuhusu ukweli** Yesu alisema:

*"Tena mmesikia walivyoambiwa watu wa zamani kwamba, 'Usiape kwa uongo, bali timiza kiapo kile ulichofanya kwa Bwana.' Lakini mimi nawaambia, msiape kabisa: iwe kwa mbingu, kwa kuwa ni kiti cha enzi cha Mungu ... 'Ndiyo' yenu iwe 'Ndiyo,' na 'Hapana' yenu iwe 'Hapana.' Lolote zaidi ya hili latoka kwa yule mwovu."*

(Mathayo 5:33-34, 37)

**Kuhusu kuwapenda watu wengine** Yesu aliweka kiwango tofauti na kile tunachokuwa nacho kwa kawaida:

*"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende jirani yako na umchukie adui yako.' Lakini ninawaambia: Wapendeni*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 26 27-05-2022 12:48:01

*adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi, ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Kama mkiwapenda tu wale wanaowapenda, mtapata thawabu gani? Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo? Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo? Kwa hiyo kuweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu."* (Mathayo 5:43-48 )

**Kuhusu utauwa na maombi** anatutahadharisha:

*"Angalieni msitende wema wenu mbele ya watu ili wawaone. Kwa maana mkifanya hivyo, hamna thawabu kutoka kwa Baba yenu aliye mbinguni.*
*Hivyo mnapowapa wahitaji, msipige panda mbele yenu kama wafanyavyo wanafiki katika masinagogi na mitaani, ili wasifiwe na watu. Amin nawaambia wao wamekwisha kupokea thawabu yao. Lakini ninyi mtoapo sadaka, fanyeni kwa siri, hata mkono wako wa kushoto usijue mkono wako wa kuume unachofanya, ili sadaka yako iwe ni siri. Ndipo Baba yako wa mbinguni, yeye aonaye sirini atakupa thawabu kwa wazi.*
*Nanyi msalipo, msiwe kama wanafiki, maana wao hupenda kusali wakiwa wamesimama katika masinagogi na kando ya barabara ili waonekane na watu. Amin nawaambia, wao wamekwisha kupata thawabu yao. Lakini wewe unaposali, ingia chumbani mwako, funga mlango na umwombe Baba yako aliye sirini. Naye Baba yako aonaye sirini atakupa thawabu yako. Nanyi mnaposali msiseme maneno kama wafanyavyo watu wasiomjua Mungu. Kwa maana wao hudhani kwamba watasikiwa kwa sababu ya wingi wa maneno yao. Msiwe kama wao, kwa sababu Baba yenu anajua kile mnachohitaji kabla hamjamwomba. Hivi basi, ndivyo iwapasavyo kuomba:*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 27 27-05-2022 12:48:01

*'Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe. Ufalme wako uje. Mapenzi yako yafanyike hapa duniani kama huko mbinguni. Utupatie riziki yetu ya kila siku. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tulivyokwisha kuwasamehe wadeni wetu. Usitutie majaribuni, bali utuokoe kutoka kwa yule mwovu [kwa kuwa Ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amen].'*
*Kwa kuwa kama mkiwasamehe watu wengine wanapowakosea, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia. Lakini msipowasamehe watu wengine makosa yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."*
(Mathayo 6:1-15)

Yesu pia anasisitiza uhusiano ulioko kati ya msamaha na maombi:

*"Nanyi kila msimamapo kusali, sameheni mkiwa na neno na mtu, ili naye Baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu."* (Mark 11:25)

Alifunza pia **kuhusu kutegemea kwetu kwa Mungu** – na utayari wa Mungu kutujibu

*"Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa mlango. Kwa kuwa kila aombaye hupewa; naye kila atafutaye hupata; na kila abishaye hufunguliwa mlango. Au ni nani miongoni mwenu ambaye mwanawe akimwomba mkate atampa jiwe? Au mwanawe akimwomba samaki atampa nyoka? Ikiwa ninyi basi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa vitu vizuri wale wamwombao?"* *(*Mathayo 7:7-11)

**Kuhusu kufunga** Yesu alitahadharisha:

*"Mnapofunga, msiwe wenye huzuni kama wafanyavyo wanafiki. Maana wao hukunja nyuso zao ili kuwaonyesha wengine kwamba wamefunga. Amin, amin nawaambia wao wamekwisha kupata thawabu yao kamilifu. Lakini*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 28 27-05-2022 12:48:01

*mnapofunga, jipakeni mafuta kichwani na kunawa nyuso zenu ili kufunga kwenu kusionekane na watu wengine ila Baba yenu aketiye mahali pa siri; naye Baba yenu aonaye sirini atawapa thawabu yenu kwa wazi.*

*Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo nondo na kutu huharibu, nao wevi huvunja na kuiba. Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba. Kwa sababu mahali hazina yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa.”* (Mathayo 6:16-21)

Vile vile **mambo ya faida halisi ya matendo mema,** pamoja na mtazamo wetu na majukumu yetu kuhusu matendo hayo, Yesu aliyafafanua:

*Ndipo Yesu akawaambia, “Jihadharini! Jilindeni na aina zote za choyo. Kwa maana maisha ya mtu hayatokani na wingi wa mali alizo nazo.”* (Luka 12:15)

*“Yeyote aliye mwaminifu katika mambo madogo, pia ni mwaminifu hata katika mambo makubwa, naye mtu ambaye si mwaminifu katika mambo madogo pia si mwaminifu katika mambo makubwa. Ikiwa hamkuwa waaminifu katika mali ya kidunia, ni nani atakayewaaminia mali ya kweli? Nanyi kama hamkuwa waaminifu na mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe? Hakuna mtumishi awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana sana na huyu na kumdharau yule mwingine. Hamwezi kumtumikia Mungu pamoja na Mali.”* (Luka 16:10-13)

Wasiwasi na mahagaiko ni sehemu ya maisha yetu. Yesu anatuonyesha njia bora ya kukabiliana na mambo hayo:

*“Kwa hiyo nawaambia, msisumbukie maisha yenu kwamba mtakula nini au mtakunywa nini; au msumbukie miili yenu kwamba mtavaa nini. Je, maisha si zaidi ya chakula, na*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 29 27-05-2022 12:48:01

*mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani; wao hawapandi wala hawavuni au kuweka ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, ninyi si wa thamani zaidi kuliko hao ndege? Ni nani miongoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha kwake anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi katika maisha yake?*

*Nanyi kwa nini mnajitaabisha kwa ajili ya mavazi? Fikirini maua ya shambani yameavyo. Hayafanyi kazi wala hayafumi. Lakini nawaambia, hata Solomoni katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya hayo maua. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya shambani, ambayo leo yapo na kesho yanatupwa motoni, je, hatawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani haba? Kwa hiyo msiwe na wasiwasi, mkisema, 'Tutakula nini?' Au 'Tutakunywa nini?' Au 'Tutavaa nini?' Watu wasiomjua Mungu ndio wanaoshindania hayo, lakini Baba yenu wa mbinguni anafahamu kuwa mnahitaji haya yote. Lakini utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake, na haya yote atawapa pia. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajitaabikia yenyewe. Yatosha kwa siku masumbufu yake."* (Mathayo 6:25-34)

Maisha yetu ina maamuzi mengi. Yesu anatuambia kwamba kuna uamuzi mmoja unaopita wote:

*"Ingieni kupitia mlango mwembamba, kwa maana lango ni pana na njia ni pana ielekeayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa kupitia lango hilo. Lakini mlango ni mwembamba na njia ni finyu ielekeayo kwenye uzima, nao ni wachache tu waionao."* (Mathayo 7:13-14)

Je, tunaona unafiki katika dini? Sote tunajua kuwa upo tele. Kwa hiyo Yesu alisema:

*"Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 30 27-05-2022 12:48:01

*ile, 'Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo wachafu na kufanya miujiza mingi?' Ndipo nitakapowaambia wazi, 'Sikuwajua kamwe. Ondokeni kwangu, ninyi watenda maovu!'*

*Kwa hiyo kila mtu ayasikiaye haya maneno yangu na kuyatenda, ni kama mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba. Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, na upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba. Lakini haikuanguka; kwa sababu msingi wake ulikuwa kwenye mwamba. Naye kila anayesikia haya maneno yangu wala asiyatende, ni kama mtu mjinga aliyejenga nyumba yake kwenye mchanga. Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, nao upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba, nayo ikaanguka kwa kishindo kikubwa."* (Mathayo 7:21-27)

Tatizo kubwa kuliko yote duniani ni **uhusiano uliovunjika.** Hasa uhusiano kati ya wanadamu na Mungu. Kulingana na mafundisho ya Yesu, alikuja kwa msingi wa kutupatanisha na Mungu. Alikuja pia kuponya uhusiano kati ya wanadamu. Kipekee alizungumza kuhusu uaminifu katika ndoa:

*"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Usizini.' Lakini mimi nawaambia kwamba, yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake."*
(Mathayo 5:27-28)

Akizungumzia kuhusu ubaya wa dhambi, ambayo huleta uvunjikaji wa mahusiano, Yesu anatumia mfano mkali:

*"Jicho lako la kuume likikusababisha kutenda dhambi, ling'oe ulitupe mbali. Ni afadhali kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako kuliko mwili wako mzima ukatupwa jehanamu. Kama mkono wako wa kuume ukikusababisha kutenda dhambi, ukate, uutupe mbali. Ni afadhali kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako kuliko mwili wako mzima utupwe jehanamu."* (Mathayo 5:29-30)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 31 27-05-2022 12:48:01

**Talaka** ni swala ambalo Yesu alizungumzia kwa msisitizo mkubwa:

*Akawajibu, "Je, hamkusoma kwamba hapo mwanzo Muumba aliwaumba mwanaume na mwanamke, naye akasema, 'Kwa sababu hii mwanaume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja'? Hivyo si wawili tena, bali mwili mmoja. Kwa hiyo alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe."* (Mathayo 19:4-6)

*"Pia ilinenwa kwamba, 'Mtu yeyote amwachaye mkewe sharti ampe hati ya talaka.' Lakini mimi nawaambia, yeyote amwachaye mkewe isipokuwa kwa kosa la uasherati, amfanya mkewe kuwa mzinzi. Na yeyote amwoaye yule mwanamke aliyeachwa, anazini."* (Mathayo 5:31-32)

*"Mtu yeyote amwachaye mkewe na kumwoa mwanamke mwingine anazini, naye mwanaume amwoaye mwanamke aliyetalikiwa anazini."* (Luka 16:18)

*Yesu akawajibu, "Musa aliwaruhusu kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu. Lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo. Mimi nawaambia, yeyote amwachaye mkewe isipokuwa kwa sababu ya uasherati naye akaoa mke mwingine, anazini. Naye amwoaye yule mwanamke aliyeachwa pia anazini."* (Mathayo 19:8-9)

Yesu anataka tuwasamehe wenzetu. Hili ni muhimu ikiwa nasi tunataka **msamaha kutoka kwa Mungu.** Yesu alitufunza jinsi ya kuomba:

*"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tulivyokwisha kuwasamehe wadeni wetu."* (Mathayo 6:12)

Pia alisema:

*"Kwa hiyo, jilindeni. Kama ndugu yako akikukosea mwonye, naye akitubu, msamehe. Kama akikukosea mara saba*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 32 27-05-2022 12:48:02

*kwa siku moja na mara saba kwa siku moja akaja kwako akisema, 'Ninatubu,' msamehe."* (Luka 17:3-4)

Mmoja wa wafuasi wa Yesu alipomwuliza, ni mara ngapi amsamehe ndugu yake, akataja: "Mara saba?" Yesu akajibu:

*"Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini."*
Mathayo 18:22

Kwa matendo yake, Yesu alithibitisha maneno yake. Mfano mzuri umeandikwa kuhusu suala hili. Lazima tusimulie hata habari zinazotangulia, siyo tu maneno aliyosema Yesu, ili kubainisha roho yake ya msamaha:

*Lakini Yesu akaenda katika Mlima wa Mizeituni. Alfajiri na mapema Yesu akaja tena Hekaluni, watu wote wakakusanyika, akakaa akaanza kuwafundisha. Walimu wa sheria na Mafarisayo wakamleta mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini. Wakamsimamisha katikati ya umati wa watu wote. Wakamwambia Yesu, "Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa akizini. Katika sheria, Mose alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, mpaka wafe. Sasa wewe wasemaje?" Walimuuliza swali hili kama mtego ili wapate sababu ya kumshtaki.*

*Lakini Yesu akainama akaanza kuandika ardhini kwa kidole chake. Walipoendelea kumuulizauliza akainuka, akawaambia, "Kama kuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe." Akainama tena na kuandika ardhini.*

*Waliposikia haya, wakaanza kuondoka mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu akabaki peke yake na yule mwanamke akiwa amesimama mbele yake. Yesu akainuka na kumwambia, "Wako wapi wale waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?"*

*Yule mwanamke akajibu, "Hakuna hata mmoja Bwana."*

*Yesu akamwambia, "Hata mimi sikuhukumu. Nenda zako, kuanzia sasa usitende dhambi tena."* (Yohana 8:1-11)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 33 27-05-2022 12:48:02

Sote tunajua kwamba Mungu anachukia dhambi. Lakini je tumetambua pia jinsi Yesu alivyokuwa na huruma kwa watenda dhambi, kama vile kifungu hiki kinavyoonyesha? Hamna cha kufananisha nacho. Yesu anangoja kila mmoja wetu aje kwake na aombe msamaha. Baada ya kupata msamaha huo, upendo wetu na shukurani yetu kwake itafanya iwe rahisi sisi kuepukana na dhambi.

Utiifu na kujitolea hakutuelekezi kwenye utumwa bali kwa uhuru kamili:

> *Kisha Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, "Kama mkidumu katika maneno yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru."* (Yohana 8:31-32)

> *Yesu akajibu, "Amin, amin nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi."* (Yohana 8:34)

Yesu aliongea kuhusu hali isiyo ya dunia hii kwenye kumwamini na kumfuata yeye:

> *Yesu akamjibu, "Amin, amin nakuambia, hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara ya pili."* (Yohana 3:3)

Akiendelea Yesu aliongeza kwamba hakuna mtu awezaye kuingia katika ufalme wa Mungu bila kupitia uzoefu wa aina hiyo. Hii inaashiria kwamba, jinsi ambavyo maisha ya kawaida huanza kwa kuzaliwa, vile vile maisha ya kiroho huanza kwa kuzaliwa kiroho. Maisha ya kiroho huanza pale "tunapowekwa huru" au "kuzaliwa upya". Tunawekwa huru baada ya Mungu kutusamehe dhambi zetu na kwa jinsi hiyo kutusafisha dhambi. Hapo basi ule utumwa umevunjika, hatia yetu imetolewa na "maisha mapya", yaani kazi ya Roho wa Mungu ndani yetu inasababisha kuwa nia zetu zinaendelea kufanywa upya (Warumi 12:2). Jambo hili hutufanya tuchukie dhambi, tupende haki, na tumfuate yule aliyetuweka huru, yaani Yesu – Masihi. Yote inaanza na uamuzi wa kukubali zawadi



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 34 27-05-2022 12:48:02

ya Mungu – msamaha wake. Matokeo yake ni kiu cha kutaka kumjua Mungu zaidi. Hiyo hufanyika tunampomruhusu Mungu azungumze nasi kupitia kwa Neno lake na kuishi kwa karibu na Baba yetu aliye mbinguni.



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 35 27-05-2022 12:48:02

## CHANGAMOTO

Ujumbe wa nabii Isa daima umekuwa changamoto kwa wanadamu. Ni changamoto ya kibinafsi tunayohitaji kuitikia. Kwa kuwa haiwezakani kutenganisha ujumbe na mjumbe, tunakabiliwa na na swali linaloamua maisha yetu yote: Je, tuko tayari kukubali ujumbe huu jinsi ulivyo na kumpokea Mjumbe jinsi anavyojitambulisha, yaani kama ufunuo wa Mungu?

Bila shaka hii inakinzana na yale ambayo Wayahudi, Waislamu, na hata Wakristo wa kijina wanayaamini. Hata hivyo, Kweli haitegemei maoni, mila, au malezi. Kwa mfano, kuna dai kuwa Yesu alisulubiwa akafa kama kafara kwa ajili ya dhambi zetu, ilhali kuna dai lingine pia kwamba Yesu hakusulubiwa wala hakufa. Madai haya mawili yote hayawezi kuwa kweli. Ikiwa moja ni kweli, "lingine" lazima liwe ni uongo.

Jibu sahihi kwa swali hilo bila shaka lo lote ndilo jambo muhimu sana katika maisha yetu. Jibu hilo ndilo linaamua maisha yetu ya milele, na hivyo ubora wa ya maisha yetu sasa. Tunashauriwa vema tusiyachukulie tu yale ambayo tamaduni au dini zetu huamuru, kama jambo la hakika, wala tusitegemee hisia zetu, na hata vibaya zaidi, tusitegemee maoni ya watu wengine.



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 36 27-05-2022 12:48:02

## THIBITISHO

Je, kuna ukweli wa kutegemewa unaoweza kuthibitisha suala hili? Ikiwa Mungu anadai tuwajibike kwa jinsi tunavyogundua na kuchagua ukweli kumhusu yeye na sisi, basi tunaweza kutarajia kwamba atatupa taratibu za kutuwezesha kutofautisha kati ya ufunuo wa kiungu na ule wa uongo.

Ili tufanye uamuzi sahihi, tunahitaji kiasi cha msingi cha utambuzi na ufahamu, na yale tunayotambua na kuyafahamu ni sharti tuyapime na kuyatumia vizuri bila upendeleo, kwa usahihi na hekima. Mawazo ya awali si vitendea kazi vizuri vya kutofautisha kati ya ukweli na ubatili.

Tumshukuru Mungu, ametupa ushahidi wa kubainisha "Kweli Yake". Ushahidi huu unapatikana kwa wote wanaojali kuutafuta:

> *Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.* (Yeremia 29:13)

Kwenye ujumbe wake kwa Musa (Kumbukumbu 18:21-22), na baadaye kupitia kwa manabii wengi (Isaya 41:21, Amosi 3:7, Yeremia 28:9), Mungu alitoa ushahidi tosha kwamba yeye ndiye mwandishi. Ushahidi huo hakuna anayeweza kuiga: Mungu alitabiri matukio yasiyoweza kutarajiwa na jinsi yatakavyotimia. Matukio ya kihistoria yasiyobashirika yalitabiriwa kwa usahihi katika Kitabu kimoja tu, nacho ni Biblia. Mara baada ya hayo kutimizwa, yalitoa thibitisho kwamba kitabu hicho kimeandikwa kwa mamlaka ya kiungu. Musa, Daudi, Isaya na wengine walitabiri kwa undani kuja na maisha ya Masihi Yesu miaka 750, 1000 na hata zaidi kabla ya kuzaliwa kwake. Ni juu yetu kuzingatia jambo hili.

Unabii huu, ambao ni wa kipekee katika kila hali, ulipotimia katika Yesu, ilikuwa dhahiri kwa ye yote aliyejali kuchunguza, kwamba ulitoka kwa Mungu. Unabii huo ulisema kwamba,



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 37 27-05-2022 12:48:02

Yesu ni *Mungu pamoja nasi* na kwamba alizaliwa na bikira (Isaya 7:14, Mathayo 1:23). Unabii huo unasema pia atakuwa *Mshauri wa Ajabu,* ***Mungu*** *Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani* (Isaya 9:6). Na kwa hiyo akawa Mwokozi wao ('Jeshua' katika Kiebrania. Ndilo jina hilo **Yesu** alijulikana nalo na wale walioishi enzi zake).

> *... akawaokoa. Katika upendo wake na rehema zake aliwakomboa watu wake.* (Isaya 63:7-9)
>
> *Lakini waliasi, na kumhuzunisha* ***Roho Mtakatifu*** *wake.* (Isaya 63:10)

Mwisho wa uasi huu ulikuwa kumkana Yesu na kuuawa kwake kulikotabiriwa katika Isaya 53:3-12 na Zaburi 22:14-18, ambapo tunasoma:

> *Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso.Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu.*
>
> *Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulidhania kuwa amepigwa na Mungu, akapigwa sana naye, na kuteswa.*
>
> *Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu; adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.*
>
> *Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, naye Bwana aliweka juu yake maovu yetu sisi sote.*
>
> *Alionewa na kuteswa, hata hivyo hakufungua kinywa chake; aliongozwa kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya wao wamkataye manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake.*
>
> *Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa. Nani awezaye kueleza kuhusu kizazi chake? Kwa maana alikatiliwa mbali*



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 38 27-05-2022 12:48:02

*na nchi ya walio hai, alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu.*

*Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu, pamoja na matajiri katika kifo chake, ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*

*Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Bwana kumchubua na kumsababisha ateseke. Ingawa Bwana amefanya maisha yake kuwa sadaka ya hatia, ataona uzao wake na kuishi siku nyingi, nayo mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake.*

*Baada ya maumivu ya nafsi yake, ataona nuru ya uzima na kuridhika; kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki, naye atayachukua maovu yao.*

*Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu, naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu, kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti, naye alihesabiwa pamoja na wakosaji. Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji.* (Isaya 53:3-12)

*Nimemiminwa kama maji, mifupa yangu yote imetoka katika viungo vyake. Moyo wangu umegeuka kuwa nta, umeyeyuka ndani yangu.*

*Nguvu zangu zimekauka kama kigae, ulimi wangu umegandamana na kaakaa la kinywa changu, kwa sababu umenilaza katika mavumbi ya kifo.*

*Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira, wametoboa mikono yangu na miguu yangu.*

*Naweza kuhesabu mifupa yangu yote, watu wananikodolea macho na kunisimanga.*

*Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura.* (Zaburi 22:14-18)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 39 27-05-2022 12:48:02

Hizi ni baadhi tu ya utabiri mwingi uliotimizwa katika Yesu. Ni zaidi ya kweli za kimantiki au hoja inayothibitisha usahihi wa Biblia. Unabii huu umebeba ujumbe. Ndani ya huu unabii Mungu anaufunua na kuuonyesha upendo wake kwetu. Ni lazima tutaitikia kwa huo upendo kwa njia moja au nyingine. Ingewezekana tutauchukia, au hatutaujali, au tutavutiwa nao. Ujumbe wa Yesu unatuita tumgeukie kwa upendo.

Kumbuka Yesu alisema:

*Tazama! Nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu yeyote akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani...*
(Ufunuo 3:20)



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 40 27-05-2022 12:48:02

## JE, UTAMKUBALI AINGIE?

Ndugu msomaji, labda moyoni na akilini mwako bado ungali na maswali kadhaa. Ikiwa ni maswali ya kutaka ufahamu, yanahitaji kujibika na yatajibika. Sisi, kama Life Challenge, tuko tayari kukusaidia kwa njia yo yote ile tuwezavyo. Sisi si wawakilishi wa Kanisa wala dhehebu lo lote, bali sisi ni waumini tunaompenda na kumheshimu Mungu na Neno lake.

Ili kukusaidia upate kuelewa Biblia kimsingi, kimetungwa kijitabu kidogo kiitwacho “Al-Kitab”. Kijitabu hiki kinapatikana katika lugha kadhaa tofauti.

Ikiwa wewe ni Mwislamu na unakabiliana na masuala kama, “Mwana wa Mungu”, “Injili ya Barnaba”, madai yasiyothibitishwa kwamba Biblia imebadilishwa, au masuala mengine kama hayo, tafadhali tuandikie ili upate bure kijitabu kiitwacho ‘Mpendwa Abdullah’.



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 41 27-05-2022 12:48:02

**Ndugu Msomaji**

Ujumbe unaoweza kutusaidia ni ule tu ambao umeeleweka.

Tafadhali chukua muda utafakari maswali yafuatayo. Utapata kijitabu kingine bure kama ukiyajibu maswali yafuatayo na kututumia majibu yako.

1. Ni "tendo" lipi muhimu sana ambalo Mungu anatarajia mwanadamu kulifanya?
2. Yesu ana ujumbe gani kwa watu ambao wamechoka na maisha?
3. Tunawezaje kujua ikiwa ujumbe wa Yesu ni wa kuaminika au la?
4. Toa sababu kwa nini kifo cha Yesu hakikuwa ajali isiyotarajiwa, bali kilikuwa katika mipango ya Mungu.
5. Kwa nini haitoshi kumkubali Yesu kama nabii tu miongoni mwa manabii wengine?
6. Yesu alithibitshaje kwamba anawapenda wanadamu?
7. Ni amri gani ya mwisho ambayo Yesu aliwapa wafuasi wake?
8. Ni nini umuhimu wa sifa "Mwana wa Adamu"?
9. Tunaweza kujifunza nini kutokana na ule mfano wa "Mwana mpotevu"?
10. Mtu mmoja aliuliza ikiwa Mafarisayo waliotajwa katika Biblia walikuwa Waislamu. Wewe utajibuje?
11. Taja baadhi ya tofauti zilizoko jinsi Waislamu wanavyoomba na jinsi Yesu alivyofunza kuhusu maombi.
12. Je, lipi ni thibitisho la kipekee kuhusu ufunuo wa Mungu kwa manabii?

Ikiwa kuna njia nyingine ile tunayoweza kukusaidia katika jitihada zako za kutafuta ukweli, tafadhali usisite kuwasiliana nasi.

Asante



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 42 27-05-2022 12:48:02

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu Mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo Wako

Al-Kitab - Kitabu cha Vitabu (kozi ya Biblia kwa njia ya posta)

*Tafadhali nitumie* ................................................................

....................................................................................

....................................................................................

....................................................................................

Tuma barua yako kwa:

Hamasa ya Milele
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

Life Challenge
P.O. Box 50770 - 00200
Nairobi, KENYA
info@life-challenge.org



05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 43 27-05-2022 12:48:02

05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 44 27-05-2022 12:48:02

05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 45 27-05-2022 12:48:02

05-MtuMwenyeUjumbe-Swahili-Edited by SB.48pages.05.22.indd 46 27-05-2022 12:48:02